



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO



Unapojibu tafadhali taja:-

Kumb. Na. DED/NMT/C.50/747

08 Novemba, 2021

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kupitia Kibali cha ajira mbadala chenye Kumb. Na.FA.170/367/01 "TEMP"/46 cha tarehe 07 Oktoba, 2021 kilichotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Anatangaza nafasi za kazi kwa wananchi wa Tanzania wenye sifa na ujuzi wa kujaza nafasi zifuatazo:-

**1: Mtendaji wa Kijiji Daraja la III (Nafasi 1)**

**(a) Sifa za Mwombaji:**

- Awe amehitimu Kidato cha nne au sita na cheti cha mafunzo (NTA LEVEL 5) katika fani mojawapo kati ya hizi; - Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii (Sociology). Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka katika Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**(b) Kazi na majukumu ya Mtendaji wa Kijiji Daraja III**

Mtendaji wa Kijiji atatekeleza majukumu yafuatayo:-

- Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia ulinzi na usalama wa Raia na Mali zao,
- Mlinzi wa Amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji,

- Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo kijijini,
- Katibu wa Mikutano Mkuu na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji,
- kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu za Serikali katika ngazi ya Kijiji.

**(c) Ngazi ya Mshahara:**

- Mwombaji atakaefanikiwa kuajiriwa kwa Cheo cha Mtendaji wa Kijiji Daraja la III atalipwa mshahara ngazi ya **TGS B** kwa mwezi.

**4: MASHARTI YA JUMLA**


- Barua za maombi ziambatishwe na nakala za vyeti vya Elimu, Taaluma, Cheti cha kuzaliwa Cheti au namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) vilivyothibishwa na Wakili au Mahakama,
- Mwombaji ambatishe Picha mbili za rangi (Passport Size) za hivi karibuni,
- Kwa wale waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe kwamba vyeti vyao vimehakikiwa na kuthibitishwa na Mamlaka (TCU au NECTA) kulingana na ngazi ya cheti,
- Maombi yaambatishwe na maelezo binafsi (CV),
- Mwombaji awe na umri wa miaka 18 hadi 45

Mwombaji mwenye sifa anatakiwa kutuma maombi kupitia Posta kwa anuani ifutayo;-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya Namtumbo,  
S. L. P 55,  
NAMTUMBO.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 21/11/2021 saa tisa Alasili.

**NB:** Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri [www.namtumbodc.go.tz](http://www.namtumbodc.go.tz)

  
Ambokile Paul

Kny: Mkurugenzi Mtendaji (W)

**NAMTUMBO**

